HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU

Mkoa wa Simiyu
Tel.Na: +255 755 820 493/
+255 625 973 343
E-mail: fugo_dox@yahoo.co.uk

Ofisi ya Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Kimali,
S.L.P 92,
MEATU - SIMIYU.

Kumb. Na: HWM/KSS/JI/VOL.I/2021 14/12/2020

Jina la Mwanafunzi:

…….....

S.L.P 44,

MEATU – SIMIYU.

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA (I) KWA MWAKA WA MASOMO 2021 KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIMALI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) 2021 katika Shule ya Sekondari **Kimali**.

Shule hii ni ya Serikali, kutwa na mchanganyiko (wavulana & wasichana) hivyo utahitajika kujitegemea kwa chakula na malazi, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu kwa muda wote wa masomo.

Shule ipo katika Tarafa ya Kimali, Kata ya Mwanhuzi, kijiji cha **Mwambegwa**, kitongoji cha **Budakama**, umbali wa kilomita 3 Magharibi kutoka mji wa Mwanhuzi (Makao makuu ya wilaya - Meatu).

Shule itafunguliwa rasmi tarehe **11/01/2021** tayari kwa Usajili na kuanza masomo, hivyo unatakiwa kufika siku hiyo bila kukosa saa **1:15** Asubuhi baada ya kukamilisha masharti na taratibu zote kama zilivyoelezwa kwenye kipengele [A] mpaka [F]. Kama hutakuwa umefika shule hadi **15/01/2021**, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yako zikiwemo pamoja na kufikishwa mahakamani mara moja.

NB: Shule pia inatoa huduma ya Hosteli/Makambi kwa wanafunzi wanaohitaji kuishi shuleni. Taratibu na mahitaji ya Makambi zitatolewa rasmi baada ya kufungua shule.

Tanbihi: Nafasi hii uliyoipata ni fursa na muhimu sana katika maisha yako ya baadae na ulimwengu wa sasa. Hivyo, unapaswa kuitumia vyema na kutoipoteza bure.!!! Kumbuka: ***"Elimu ni Ukombozi"***

Nakutakia maandalizi mema na Karibu sana.

……..

JOSEPH M. FUGO
MKUU WA SHULE.

HEADMASTER
KIMALI SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 92
MWANHUZI

Nakala:

1. Mkurugenzi Mtendaji (W),
   MEATU – SIMIYU. Kwa Taarifa.

MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE:

[A]: SARE ZA SHULE (SCHOOL UNIFORMS):

(i). WAVULANA:

- Suruali mbili (02) ndefu rangi ya Dark blue.
- Mashati mawili (02) meupe ya tetron mikono mifupi yasiyobana na kushika pasi.
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vinavyong'arishwa na kiwi jozi moja (01).
- Soksi dark blue/nyeusi jozi mbili (02).
- Viatu vya michezo (raba jozi moja)
- Bukta moja (01) ya Blue kwa ajili ya michezo.
- Fulana (T-shirt) moja (01) yenye kola shingoni na Nembo ya Shule rangi ya 'damu ya mzee' kwa ajili ya michezo na shughuli za nje.
- Tai moja (01) rangi ya Dark blue. Na sweta moja (01) dark blue kwa ajili ya kujikinga na baridi.

(ii). WASICHANA:

- Sketi mbili (02) **ndefu kufunika miguu yote** rangi ya Dark blue.
- Mashati mawili (02) meupe ya tetron mikono mifupi yasiyobana na kushika pasi. Kwa wasichana waislam, watavaa mashati meupe mikono mirefu na Ushungi/vijuba rangi nyeupe.
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vinavyong'arishwa na kiwi jozi moja (01).
- Soksi ndefu (stoking) nyeupe jozi mbili (02).
- Suruali ya Track moja (01) ya Blue kwa ajili ya michezo.
- Fulana (T-shirt) moja (01) yenye kola shingoni na Nembo ya Shule rangi ya 'damu ya mzee' kwa ajili ya michezo na shughuli za nje.
- Skafu moja (01) rangi ya Dark blue. Na sweta moja (01) dark blue kwa ajili ya kujikinga na baridi.

Tanbihi: Unatahadharishwa kuwa **Suruali** na **Sketi** utakazoshona, ni lazima ziwe ***ndefu*** na ***marinda***.
Pia suruali kwa chini ni lazima ziwe na pindo. Suruali za ***mode***l na Sketi ***zinazobana (tight)*** **HAZIRUHUSIWI** na hautapokelewa kamwe katika shule hii.

[B]: VIFAA VYA KUJIFUNZIA

- Daftari kubwa (Counter books 4 Quire au 3 Quire) za kuandikia Nukuu za Masomo = 13
- Kalamu za blue/nyeusi = 2
- Kofa (Mathematical Set) = 1
- Rula ndefu (sentimita 30) = 1
- Kamusi ya Kiingereza (English Dictionary) = 1

[C]: KARO YA SHULE NA MICHANGO MINGINE:

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, (2015 - 2020) Ibara ya 52 (a) imebainisha kwamba Serikali itatoa elimu ya awali na elimumsingi (darasa la I hadi Kidato cha 4) bila malipo kuanzia mwaka wa masomo 2016. Hivyo **HAPATAKUWA** na ulipaji wa Ada na michango mengine ya shule. Serikali itagharamia michango hiyo.

[D]. MEDICAL EXAMINATION (VIPIMO VYA AFYA):

Utalazimika kupimwa na Mganga wa Hospitali ya Serikali (Wilaya) ili kuthibitisha Afya yako kama inaruhusu kumudu masomo ya Sekondari. Nenda Hospitali ukiwa na Fomu 'F' iliyoambatanishwa, kisha njoo nayo na uikabidhi mara ufikapo shuleni, ukiwa na taarifa zinazotakiwa toka kwa Mganga wa Serikali.

[E]: SHERIA ZA SHULE:

Utasomewa Sheria na Taratibu za shule mara tu ufikapo shuleni na itabidi uzielewe na kuzifuata kikamilifu.

Tanbihi: Hakikisha unakuja na mahitaji yote siku ya kufungua shule.

(i) Picha A

(ii) Picha B

Maelezo ya ziada juu ya Ushonaji wa Sketi:

1. Sketi ni **lazima** iwe ndefu kufunika miguu yote kama inavyoonekana hapo juu.
2. Sketi iwe flat (isiwe na marinda) sehemu ya mbele na nyuma kama inavyoonekana kwenye **picha A**.
3. Sketi iwe na size ya marinda pembeni (mguu wa kulia na kushoto) kama inavyoonekana kwenye **picha B**.
4. Sketi iwe na michirizi miwili meupe ya riboni katikati ya sehemu ya flat ya mbele.

……..

JOSEPH M. FUGO

MKUU WA SHULE.

HEADMASTER
KIMALI SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 92
MWANHUZI

[F]: STUDENT MEDICAL CERTIFICATE:

Name of Student: _____ Sex: _____ Age: _____

(To be completed by a government Medical Officer and returned to the **Headmaster, Kimali Secondary School, P.O.BOX 92, MEATU - SIMIYU**).

Please examine the Student named above and comment of his/her health by responding to the following items: Kindly put a tick (√) in front of each item either YES or NO.

Does the student have problems in connection with;

(a) Sight? …… 1. NO

2. YES

If yes state:……...

(b) Hearing? ……..….. 1. NO

2. YES

If yes state:……...

(c) Speech? …….. 1. NO

2. YES

If yes state: ……..

(d) T.B. ? …….. 1. NO

2. YES

If yes state: ……..

(e) Blood pressure? ……..…. 1. NO

2. YES

If yes state: ……..……

(f) Any physical disability? …… 1. NO

2. YES

If yes state: ……..……

(g) Any other health problems e.g. Pregnancy, STDs. ……... 1. NO

2. YES

If yes state: …….

(h) Do you therefore recommend the said student medically fit, for student-ship at this school?

…… 1. NO

2. YES

If NO, please state: …….....

.....

…….. ……

Name and Signature **Designation**

Date: …… Official stamp: ……